SAU

SAUTI YA UMMA
(PEOPLE'S VOICE)

# KATIBA
# YA
# CHAMA CHA SAU

## TOLEO LA 2010

SAU

SAUTI YA UMMA
(PEOPLE'S VOICE)

# KATIBA
# YA
# CHAMA CHA SAU

**TOLEO LA 2010**

# CHAMA CHA SAUTI YA UMMA (SAU)
# KATIBA

## TOLEO LA 2010

## YALIYOMO


| | | | |
|---|---|---|---|
| 1.0 | SURA YA KWANZA | MADHUMUNI YA CHAMA NA MAKAO MAKUU YA CHAMA | UK. 1 |
| 2.0 | SURA YA PILI | UANACHAMA | UK. 2 |
| 3.0 | SURA YA TATU | VIKAO VYA CHAMA | UK. 3 |
| 4.0 | SURA YA NNE | UTARATIBU WA UCHAGUZI MIKUTANO | UK. 9 |
| 5.0 | SURA YA TANO | MENGINEYO | UK. 10 |


## SURA YA KWANZA

JINA LA MADHUMUNI.

1.0 JINA

1.1 Jina la Chama litakuwa
SAU

**2.0 MAKAO MAKUU YA CHAMA**

2.1 Makao Makuu ya Chama yatakuwa Dar es Salaam

2.2 Patakuwa na Ofisi Ndogo ya Makao Makuu huko Zanzibar ambayo itaratibu shughuli za Chama Tanzania Zanzibar.

2.3 Bendera: Bendera ya SAU itakuwa ya rangi ya Bluu bahari, mkanda mweusi katikati, Nyeupe pembeni yenye nembo ya mkono wenye Vidole Vitano na maneno yaliyoandikikwa SAU, Sauti ya Umma (People's Voice

**3.0 MADHUMUNI**

**Madhumuni ya Chama ni:-**

3.1 Kisiasa

3.1.1 Kukuza, kulinda na kutetea haki za binadamu katika misingi ya Tangazo ya Ulimwengu na Haki za Binadamu na mikataba yote ya Kimataifa inayolinda haki hizo na inayofuatilia mbalimbali ukandamizwaji wa watu katika misingi ya rangi, jinsia, kabila, dini au tabaka

3.1.2 Kuhakikisha kila mtu ana haki na uhuru wa kuabudu kwa minajili ya dini, madhehebu au imani yoyote anayotaka, bila kuathiri amani na / au utulivu wa jamii.

3.1.3 Kuendeleza na kudumisha Demokrasia kwa kushirikisha vyama vingi vya siasa, kujenga utamaduni wa demokrasia katika jamii kwa kutambua haki za wengi katika maamuzi na pia kukubali haki za wachache kusikilizwa, kuheshimiwa na kulindwa na kukubali ushindani huru wa haki na wa wazi katika uchaguzi.

3.1.4 Kuhakikisha kila mtu ana uhuru wa kwenda mahali popote ndani ya mipaka ya nchi na kwamba anaweza kushirikiana na mtu yeyote ndani na nje ya nchi katika kuendeleza maslahi halali ya washirika na kuwa kuna uhuru wa kukutana na kuandamana kwa amani ili kuendeleza hayo maslahi.

3.1.5 Kudumisha uhusiano wa kirafiki wa mataifa duniani, Afrika na nchi jirani, kuyaheshimu maazimio yote ya kimataifa kwa kulingana na kanuni zilizopo za kimataifa na Katiba ya Umoja wa Mataifa.

**3.2 Kiuchumi**

3.2.1 Kukuza na kuimarisha uchumi wa nchi kwa kutumia rasilimali za nchi yetu kwa uwezo walionao wananchi bila kuathiri uhuru wa Taifa na kuhakikisha kuwa jamii kwa ujumla inanufaika.

3.2.2 Kujenga na kuimarisha uchumi wa soko huru, utakaoheshimu na kulinda haki na mali za watu, biashara huru na sekta ya watu binafsi na pale inapobidi kutoa nafasi kwa sekta ya Umma.

3.2.3 Kujenga na kuimarisha kilimo na ufugaji katika lengo la kutosheleza Taifa kwa chakula na mazao ya biashara; kuboresha wakulima na wafugaji na kuendeleza sera ya kulinda ardhi, maliasili na mazingira kwa manufaa ya wananchi.

3.2.4 Kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali za nchi ili zichangie kikamilifu katika pato la Taifa.

3.2.5 Kujenga misingi ya ajira ya hali ya juu na kuongeza uwezo wa wananchi kujiajiri wenyewe, na kuhakikisha kipato kinalingana na jasho au juhudi za muajiriwa.

3.2.6 Kutoa mkazo katika Utafiti, Sayansi na Teknolojia ili kuchochea mipango ya maendeleo ya Taifa.

nchini kwa lengo la uzalishaji wa bidhaa kwa matumizi ya ndani na biashara ya nje.

3.2.8 Kuimarisha sekta ya usafiri na mawasiliano muhimu hususan, barabara, reli, bandari, ndege, simu televisheni, radio, magazeti na njia zingine zozote za mawasiliano.

**3.3 KIJAMII**

3.3.1 Kuendeleza juhudi za kuhakikisha haki za wanawake na kuelimisha Umma ili kuondoa fikra na mila potofu za ukandamizaji wa jinsia pamoja na kutekeleza makubaliano na mikataba ya Kimataifa kuhusu haki za watoto.

3.3.2 Kuboresha, kutunza na kutoa huduma za jamii kwa mfano: Afya, Elimu na Usalama wa Raia, kwa ajili ya kukuza hali ya maisha ya watu.

3.3.3 Kuhifadhi na kuboresha utamaduni wa Taifa ili kujenga hadhi na heshima ya Watanzania na kuendeleza Nyanja zote za utamaduni, burudani, michezo, sanaa na historia ya nchi.

3.3.4 Kutoa huduma za kuridhisha kwa vikundi mbalimbali katika jamii hususani walemavu, watoto na wazee ambao hawapo katika mkondo wa kujipatia kipato cha kutosheleza mahitaji ya kawaida.

## SURA YA PILI

**4.0 MASHARTI YA UANACHAMA**

4.1 Mwananchi yeyote aliyefikisha umri wa miaka 18 aliye na akili timamu anayekubali, Madhumuni na Katiba ya Chama anaweza kuwa mwanachama. Mwanachama anawajibika kuwa na kadi na kulipa ada kwa mujibu wa taratibu na kanuni zitakazoamuliwa na chama.

**HAKI ZA MWANACHAMA**

4.2 (i) Kila mwanachama anayo haki ya kuchagua na kuchaguliwa katika uongozi wa ngazi yoyote katika chama.
(ii) Kutoa hoja za kusahihisha na kuweka sawa miongozo ya chama bila hofu wala upendeleo kwa kupitia ngazi husika za chama.
(iii) Haki ya kujitetea mbele za vikao vya chama vitakavyohusika na madai yoyote dhidi yake.
(iv) Haki ya kukata rufaa kwa vikao vya juu asiporidhika na uamuzi wa vikao vya chini.

4.3 (i) Kila mwanachama ana haki ya kushiriki kikamilifu katika shughuli na uongozi wa chama na kueneza sera na program ya chama.
(ii) Kujielimisha juu ya masuala ya jamii, kuelewa matatizo ya watu, kiini chake na kujitahidi kutafuta majibu ya matatizo hay kwa kushirikiana na wahusika.

**WAJIBU WA MWANACHAMA**

4.4 (i) Kila mwanachama ana wajibu wa kutetea Haki za binadamu
(ii) Kupinga uonevu, dhuluma, rushwa, ubaguzi wa kila aina na matendo yanayoharibu maadili ya utamaduni wa nchi yetu.
(iii) Kukuza moyo wa ushirikiano na kuthamini uamuzi wa pamoja na kuhudhuria vikao vya chama vinavyomhusu.
(iv) Kutekeleza maagizo yote ya viongozi na vikao vya chama.

**KUACHA UANACHAMA**

4.5 (i) Uanachama unaweza kukoma iwapo wmanachama atajiuzulu mwenyewe
(ii) Atafariki
(iii) Iwapo ataachishwa au kufukuzwa kwa mujibu wa Katiba, atakuwa na haki ya kujitetea na kuomba rufaa Kamati Kuu.

4.6 Mwanachama atafukuzwa au kuachishwa uanachama iwapo:-

kitendo cha kujiunga na Chama kingine cha Siasa.

(ii) Bila kuathiri haki za mwanachama chini ya Sheria za nchi kitendo cha kumfukuza au kumwachisha uanachama mwanachama yeyote kitachukuliwa na Kamati Kuu pekee baada ya kupata mapendekezo kutoka ngazi za chini.

Mwanachama aliyeachishwa au kufukuzwa anaweza kurejea chamani kwa kuomba uanachama upya na kuidhinishwa na Kamati Kuu.

## SURA YA TATU

### 5.0 VIKAO VYA CHAMA

5.1 Tawi

Tawi linaweza kuanzishwa:

5.1.1 Ikiwa katika makazi ya vijijini, kuna wanachama wasiopungua 20 au
Ikiwa katika makazi ya mijini, kuna wanachama wasiiopungua 30

**Vikao vya Tawi**

5.1.3 Mkutano Mkuu wa Tawi

5.1.4. Mkutano wa Kamati ya Utendaji ya Tawi

**Mkutano Mkuu wa Tawi**

5.1.5 Mkutano Mkuu wa Tawi utahudhuriwa na wanachama wote kama wajumbe. Uhalali wa Mkutano ni theluthi mbili ya wanachama.

5.1.6 Iwapo idadi haikupatikana kwenye Mkutano. Mwenyekiti ataaihirisha mkutano kwa muda wa mwezi mmoja. Mkutano huu wa pili utaendelea iwapo wanachama wasiopungua nusu watahudhuria ieleweke kuwa mwanachama ni lazima awe amelipia kadi yake kikamilifu wakati wa mkutano.

**Majukumu ya Mkutano Mkuu wa Tawi**

5.1.7. Kuchagua Mwenyekiti wa Tawi

5.1.8. Kuchagua Mkurugenzi wa Tawi

5.1.9 Kuchagua Mkurugenzi Mwenezi wa Tawi

5.1.10 Kuchagua Mweka Hazina

5.1.11 Kuchagua Mwenyekiti wa Wanawake

5.1.12 Kuchagua Mwenyekiti wa vijana

4.1.13 Kuchagua wajumbe 5 wa Kamati Kuu ya Tawi

5.1.14 Kuchagua mjumbe 1 kuhudhuria Mkutano Mkuu wa Kata.

5.1.15 Kujadili wagombea uwenyekiti wa vijiji, vitongoji na mitaa na kuwakilisha mapendekezo yao kwa mkutano mkuu wa kata kwa uamuzi wa mwisho.

5.1.16 Kujadili taarifa za Kamati Kuu ya Tawi na kutoa uamuzi au mwongozo wa utekelzaji wa taarifa hiyo.

5.1.17 Kuzingatia na kutekeleza maagizo ya chama kutoa ngazi za juu.

5.1.18 Kujadili sera za chama zinazohusu maendeleo ya wananchi kwa jumla katika ngazi ya Tawi.

5.1.19 Mkutano Mkuu wa Tawi utafanyika siyo chini ya mara moja kwa mwaka chini ya uongozi wa Mwenyekiti wa muda atakayechaguliwa miongoni mwa wajumbe kama Mwenyekiti wa Tawi hawezi kuhudhuria.

**Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Tawi.**

5.1.20 Mwenyekiti wa Tawi

5.1.21 Mkurugenzi wa uenezi wa Tawi

5.1.23 Mweka hazina

5.1.24 Mwenyekiti wa shughuli za wanawake

5.1.25 Mwenyekiti wa shughuli za vijana

5.1.26 Wajumbe watano wa kuchaguliwa na Mkutano Mkuu wa Tawi

5.1.27 Diwani mwanachama anayoishi katika eneo la Tawi

5.1.28 Mwenyekiti – shughuli za wazee

**(Kamati inaweza kumkaribisha Mbunge, Mwakilishi au Diwani wa Chama kuhudhuria na kushiriki katika shughuli hata kama haishi katika eneo la Tawi lakini hatakuwa na haki ya kupiga kura)**

**Shughuli za Kamati ya Utendaji ya Tawi**

5.1.29 Kuendeleza shughuli za Chama za kila siku

5.1.31 Kuandaa Mkutano Mkuu wa Tawi
5.1.32 Kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya Mwanachama
5.1.33 Kamati Kuu itakutana kama inavyohitaji lakini siyo chini ya mara moja kwa mwezi.
5.1.34 Uhalali wa Mkutano utakuwa nusu ya wajumbe mradi kati yao atakuwa Mwenyekiti au Mkurugenzi.
5.1.35 Iwapo Mwenyekiti hawezi kuhudhuria wajumbe watamchagua mmoja wao kuwa Mwenyekiti wa Mkutano huo.

## 5.2 Kata

Vikao vya Chama kwenye Kata

5.2.1 Mkutano Mkuu wa Kata.
5.2.2. Mkutano wa Kamati ya Utendaji ya Kata.

**Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kata**

5.2.3 Mwenyekiti wa Chama wa Kata
5.2.4 Mkurugenzi wa Chama wa Kata
5.2.5 Mkurugenzi wa Uenezi wa Kata
5.2.6 Mweka Hazina wa kata
5.2.7 Mwenyekiti wa wanawake na naibu wake.
5.2.8. Mwenyekiti wa vijana na naibu wake.
5.2.9 Wenyeviti na Wakurugenzi wote wa Matawi katika Kata hiyo
5.2.10 Mjumbe mmoja kutoka katika kila tawi.
5.2.11 Mbunge wa Chama anayewakilisha jimbo ambapo Kata hiyo imo endapo anaishi katika Kata hiyo.
5.2.12 Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Chama wanaoishi katika Kata hiyo
5.2.13 Diwani wa Chama katika kata hiyo.
5.2.14 Mwenyekiti wa Wazee na naibu wake

**Shughuli za Mkutano Mkuu wa Kata**

5.2.15 Kusimamia, kuongoza na kutathmini utendaji wa matawi yaliyoko kwenye Kata hiyo.
5.2.16 Kupokea, kujadili na kutoa miongozo ya kiutendaji na kupokea taarifa za kamati kuu za matawi ya Kata hiyo.
5.2.17 Kubuni na kupendekeza sera za chama katika Kata
5.2.18 Kutekeleza sera na maagizo ya juu.
5.2.19 Kumchagua Mwenyekiti wa Chama wa Kata
5.2.20 Kumchagua Mkurugenzi wa Uenezi wa Kata
5.2.21 Kuwachagua wajumbe watano wa Kamati Kuu ya Kata.
5.2.22 Kuwachagua wenyeviti na manaibu wenyeviti wa wanawake na vijana
5.2.23 Kupiga kura na kuchagua wagombea uwenyekiti wa vijiji, vitongoji wa mitaa
5.2.24 Kujadili wagombea wa udiwani na kuwasilisha mapendekezo yao wilayani,
5.2.25 Kuchagua wajumbe 2 wa Mkutano Mkuu wa Wilaya
5.2.26 Halali ya Mkutano ni theluthi mbili za Wajumbe wote
5.2.27 Mkutano Mkuu wa Kata utakutana kwa kikao cha kawaida mara moja kwa mwaka.

**Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Kata**

5.2.28 Mwenyekiti wa Chama cha Kata
5.2.29 Mkurugenzi wa Chama wa Kata
5.2.30 Mkurugenzi wa Uenezi wa Kata
5.2.31 Mweka Hazina wa Kata
5.2.32 Mwenyekiti wa wanawake wa Kata
5.2.33 Mwenyekiti wea Vijana
5.2.34 Wajumbe watano waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kata
5.2.35 Wabunge na wajumbe wa Baraza la wawakilishi wa chama wanaoishi katika Kata.
5.2.36 Diwani wa Chama katika kata hiyo.
5.2.37 Mwenyekiti wa wazee.

(Kamati inaweza kumkaribisha Mbunge au Mwakilishi wa Chama wa Wilaya ambako Kata hiyo iko hata kama haishi katika Kata hiyo, lakini hatakuwa na haki ya kupiga kura).

**Shughuli za Kamati ya Utendaji ya Kata**

5.2.38 Kuendesha shughuli zote za chama za kila siku
5.2.39 Kuratibu shughuli zote za chama katika Kata
5.2.40 Kujadili sera na mipango ya chama

5.2.42 Kuteua Mweka Hazina wa Kata
5.2.43 Kumteua Mkurugenzi wa Kata.
5.2.44 Kuamua kuhusu maombi ya wanachama waliokataliwa na Tawi. Kutafakari mapendekezo kutoka Tawi kuhusu hatua za kinidhamu zilizochukuliwa na Tawi dhidhi ya mwanachama au wanachama.
5.2.45 Kuratibu shughuli za Matawi ya Chama
5.2.46 Kamati Kuu ya Kata itakutana siyo chini ya mara moja katika miezi mitatu (3)
5.2.47 Halali ya Mkutano isiwe chini ya nusu (1/2) ya wajumbe wote.
5.2.48 Iwapo Mwenyekiti hawezi kuhudhuria wajumbe watamchagua mmoja wao kuwa Mwenyekiti wa Mkutano huo.

**5.3 WILAYA**

**Vikao vya chama kwenye Wilaya**

5.3.1 Mkutano Mkuu wa Chama wa Wilaya
5.3.2 Mkutano wa Kamati ya Utendaji ya Wilaya

**Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya**

5.3.3 Mwenyekiti wa Chama wa Wilaya
5.3.4 Mkurugenzi na Naibu Mkurugenzi wa Chama Wilaya.
5.3.5 Mkurugenzi na Naibu Mkurugenzi wa uenezi wa Chama wa Wilaya
5.3.6 Mweka Hazina wa Wilaya
5.3.7 Mwenyekiti wa wanawake na naibu wake
5.3.8 Mwenyekiti wa Vijana na naibu wake
5.3.9 Mwenyekti na Wakurugenzi wote wa Kata katika Wilaya hiyo.
5.3.10 Wajumbe wa Wilaya anayehudhuria Mkutano Mkuu Taifa
5.3.11 Mbunge au Wabunge wa Chama wanaoishi au kuwakilisha Wilaya hiyo
5.3.12 Wajumbe wa Wilaya anayehudhuria Mkutano Mkuu Taifa
5.3.13 Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Chama wanaoishi au kuwakilisha Wilaya hiyo
5.3.14 Madiwani (wa Chama) wote wa Wilaya hiyo.
5.3.15 Mwenyekiti wa Halmashauri ya miji na Halmashauri ya Wilaya (wa chama)

**Shughuli za Mkutano Mkuu wa Wilaya**

5.3.16 Kusimamia, kuongoza na kutathmini Utendaji wa Matawi na kaza za Wilaya
5.3.17 Kupokea, kujadili na kutoa mwongozo wa kiutekelezaji na kupokea taarifa za Kamati Kuu ya Wilaya.
5.3.18 Kubuni na kupendekeza sera za chama kwa maendeleo ya jamii.
5.3.19 Kutekeleza sera na maagizo ya ngazi za juu za chama
5.3.20 Kutekeleza sera madhubuti za kuendeleza uhai wa chama katika Wilaya.
5.3.21 Kumchagua Mwenyekiti wa Chama wa Wilaya.
5.3.22 Kupendekeza jina la Mkurugenzi wa Wilaya Mkoani
5.3.23 Kumchagua Mkurugenzi wa uenezi wa Chama wa wilaya
5.3.24 Kuchagua wajumbe watano wa Kamati Kuu.
5.3.26 Kuchagua wajumbe wawili wa Mkutano Mkuu wa Mkoa
5.3.27 Kuchagua Mjumbe mmoja atakayehudhuria Mkutano Mkuu wa Taifa (National Conference) kulingana na utaratibu wa chama
5.3.28 Kupiga kura na kuchagua wagombea udiwani.
5.3.29 Kutoa mapendekezo yao kuhusu mwanachama baina ya wanachama wanogombea Ubunge au Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi katika Wilaya hiyo na kuyawakilisha Mkoani kwa uamuzi wa kila tawi. Uchaguzi huu utasimamiwa na Mjumbe kutoka Mkkoani au Taifa.
5.3.30 Halali ya Mkutano ni theluthi mbili ya wajumbe
5.3.31 Mkutano Mkuu wa Wilaya utakutana kwa kawaida mara moja kwa mwaka.
Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Wilaya ni:-
5.3.32 Mwenyekiti wa Chama wa Wilaya
5.3.33 Mkurugenzi na Naibu Mkurugenzi wa Chama wa Wilaya
5.3.34 Mkurugenzi wa Uenezi wa Chama
5.3.35 Mweka Hazina wa Chama
5.3.36 Mwenyekiti wa Wanawake
5.3.37 Mwenyekiti wa Vijana
5.3.38 Wajumbe watano waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Wilaya
5.3.39 Wabunge na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa chama wanaowakilisha Wilaya hiyo.
5.3.40 Mwenyekiti wa Wazee

5.3.41 Kuendesha shughuli za chama kila siku.
5.3.42 Kuratibu shughuli zote za chama Wilayani.
5.3.43 Kuandaa Mkutano Mkuu wa Wilaya ikiwa ni pamoja na kuchambua na kupeleka mkutano mkuu majina ya wanachama wanaogombea ubunge au ujumbe wa Baraza la Wawakilishi Wilaya hiyo.
5.3.44 Kuteua mweka hazina na naibu Mkurugenzi wa Wilaya.
5.3.45 Kuamua kuhusu maombi ya wanachama waliokataliwa na kata. Aidha kutafakari mapendekezo ya hatua ya kinidhamu ya kamati ya Utendaji ya kata na ikiona inafaa kupeleka mapendekezo kwenye kamati ya Utendaji ya Mkoa
5.3.46 Kamati ya Utendaji itakutana kama inavyohitajika lakini siyo chini ya mara moja kwa miezi mitatu.
5.3.47 Halali ya Mkutano ni nusu ya wajumbe.
5.3.48 Iwapo Mwenyekiti hawezi kuhudhuria wajumbe watamchangua mmoja wao kuwa Mwenyekiti wa Mkutano huo.

**5.4 MKOA**

**Vikao vya chama kwenye mkoa vitakuwa:**

5.4.1 Mkutano Mkuu wa chama wa Mkoa.
5.4.2 Mkutano wa kamati ya Utendaji ya Mkoa.

**Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkoa:**

**5.4.3 Mwenyekiti wa Chama wa Mkoa.**
5.4.4 Mkurugenzi na naibu Mkurugenzi wa chama wa Mkoa.
5.4.5 Wenyeviti na Wakurugenzi wa chama wa Wilaya.
5.4.6 Wajumbe wawili kutoka kila wilaya waliochaguliwa na mkutano Mkuu wa Wilaya
5.4.7 Mwakilishi wa Mkoa kwenye Mkutano Mkuu Taifa.
5.4.8 Mwenyekiti katika Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya ambaye niii mwanachama.
5.4.9 Wabunde na wawakilishi wanachama kutoka Mkoa huo
5.4.10 Mweka Hazina wa Mkoa
5.4.11 Mkurugenzi na Naibu Mkurugenzi wa uenezi wa Mkoa.
5.4.12 Mwenyekiti wa wanawake na naibu wake.
5.4.13 Mwenyekiti wa vijana na naibu wake.

**Shughuli za Mkutano Mkuu wa Mkoa**

5.4.14 Kusimamia, kuongoza na kutathmini Utendaji wa Chama Mkoani.
5.4.15 Kupokea na kujadili taarifa za Kamati Kuu ya Mkoa na kutoa mwongozo wa kiutekelezaji
5.4.16 Kubuni na kuratibu shughuli za chama mkoani
5.4.17 Kumchagua Mwenyekiti wa Chama wa Mkoa
5.4.18 Kupendekeza kwa Kamati Kuu majina ya Mkurugenzi wa Mkoa na Wakurugenzi wa Wilaya
5.4.19 Kumchagua Mkurugenzi wa uenezi wa chama wa Mkoa na Naibu wake.
5.4.20 Kumchagua Mjumbe mmoja kila Wilaya wa Kamati Kuu ya Mkoa
5.4.21 Kuwachagua wenyeviti na manaibu wenyeviti wa wanawake na vijana
5.4.22 Kumchagua Mjumbe mmoja atakayehudhuria Mkutano Mkuu wa chama wa Taifa.
5.4.23 Kupokea na kujadili mapendekezo ya wilaya juu ya wagombea Ubunge, Baraza la Wawakilishi kwa kuzingatia mapendekezo ya wilaya na kutoa maamuzi ya mwisho baada ya kupata uthibitisho wa Kamati Kuu.
5.4.24 Halali ya Mkutano ni theluthi mbili ya Wajumbe wa Mkutano.
5.4.25 Mkutano Mkuu wa Mkoa wa kawaida utakutana mara moja kila miaka miwili

**Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Mkoa ni;**

5.4.26 Mwenyekiti wa Chama wa Mkoa.
5.4.27 Mkurugenzi na Naibu Mkurugenzi wa Chama wa Mkoa
5.4.28 Wajumbe waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Mkoa mmoja kila Wilaya.
5.4.29 Mkurugenzi wa Uenezi na Naibu wake
5.4.30 Mweka Hazina
5.4.31 Mwenyekiti wa wanawake
5.4.32 Mwenyekiti wa Vijana
5.4.33 Mbunge au mwakilishi anayewakilisha Mkoa kwenye Bunge au Baraza la Wawakilishi
5.4.34 Mjumbe wa Mkoa anayehudhuria Mkutano Mkuu wa Taifa
5.4.35 Mwenyekiti – Wazee

**Shughuli za Kamati ya Utendaji ya Mkoa.**

5.4.36 Kuendesha shughuli zza kila siku
5.4.37 Kuratibu shughuli zote za Chama Mkoani
5.4.38 Kujadili sera na mipango ya Chama

5.4.40 Kuamua kuhusu maombi ya wanachama waliokataliwa na vikao vya chini. Aidha kutafakari mapendekezo ya hatua za kinidhamu ya Kamati ya Utendaji ya Wilaya na ikiona inafaa kupelekea mapendekezo kwenye Kamati Kuu ya Taifa.
5.4.41 Kumteua Mweka Hazina wa Mkoa.
5.4.42 Kamati ya Utendaji ya itakutana kama inavyohitajika siyo chini ya mara moja kwa kila miezi mitatu.
5.4.43 Halali ya Mkutano ni nusu ya Wajumbe, Mwenyekiti au Katibu awepo.
5.4.44 Iwapo Mwenyekiti hawezi kuhudhuria, wajumbe watamchagua mmoja wao kuwa Mwenyekiti wa mkutano huo.

## 5.5 TAIFA

Mwenyekiti Taifa na Katibu Mkuu ndio viongozi wakuu wa chama, Makamu Mwenyekiti Taifa atakaimu Unyekiti kama Mwenyekiti hayupo.

**Vikao vya chama kwenye Taifa vitakuwa**

5.5.1 Mkutano Mkuu wa Chama
5.5.2 Kamati Kuu ya Chama
5.5.3 Sekretarieti ya Kamati Kuu
5.5.4 Hakutakuwa na Baraza Kuu la Chama. Shughuli zake zitafanywa na Kamati Kuu. Mkutano mkuu wa chama utafanyika kila baada ya miaka saba na utaitishwa na Mwenyekiti Taifa ya kwa kushauriana na Katibu Mkuu.

**Wajumbe wa Mkutano Mkuu**

5.5.5 Mwenyekiti wa Chama
5.5.6 Makamu Wenyekiti wa Chama Zanzibar na Bara
5.5.7 Katibu Mkuu wa Chama
5.5.8 Manaibu Makatibu Wakuu Zanzibar na Bara.
5.5.9 Wakuu wote wa Kurugenzi Makao Makuu na Wasaidizi wao
5.5.10 Wenyeviti wa Mikoa
5.5.11 Wakurugenzi wa Mikoa (Makatibu)
5.5.12 Wajumbe wanne (wawili kutoka Zanzibar na wawili kutoka Bara) walioteuliwa na Kamati Kuu.
5.5.13 Wajumbe wanne wa fani mbalimbali walioteuliwa na Kamati Kuu.
5.5.14 Mjumbe mmoja kutoka kila Wilaya
5.5.15 Wenyeviti wote wa Wilaya
5.5.16 Wakurugenzi wote wa Wilaya (Makatibu)
5.5.17 Wabunge na Wawakilishi wa Chama na madiwani
5.5.18 Wajumbe wawili kutoka kila Jumuiya ya Chama waliochaguliwa na Mkutano Mkuu.

**Shughuli za Mkutano Mkuu wa Chama wa Taifa:**

5.5.19 Kutunga na kubadilisha, inapobidi Katiba ya Chama.
5.5.20 Kusimamia, kuongoza na kutathimini sera za chama kitaifa.
5.5.21 Kumchagua Mwenyekiti wa Chama – Taifa na Makamu wake Bara na Zanzibar.
5.5.22 Kupokea, kujadili na kutoa uamuzi au mwongozo wa kiutekelezaji kuhusu taarifa ya Kamati Kuu au kikao kingine cha Taifa, Mkoa, Wilaya, Kata au Tawi.
5.5.23 Kubuni na kupanga utekelezaji wa maendeleo ya Chama kitaifa.
5.5.24 Kuidhinisha ilani (manaifesto) ya chama kutokana na mapendekezo ya Kamati Kuu ya Chama.
5.5.25 Kujadili na kuteua wagombea Urais wa Jamhuri ya Muungano na Makamu wake wa Urais wa Zanzibar.
5.5.26 Kusikiliza na kutoa uamuzi wa mwisho unaohusu rufaa zitakazowakilishwa na Kamati Kuu ya Chama.
5.5.27 Uhalali wa Mkutano Mkuu ni theluthi mbili ya wajumbe wa Mkutano. Mkutano wa Taifa wa chama utaitishwa kila baada ya miaka saba (7) isipokuwa inapotokea dharura. Wajumbe wa Mkutano Mkuu wanaweza kupungua kutokana na uwezo wa fedha wa chama kwa kuzingatia uwiano wa mikoa.
5.5.28 Mikutano Mikuu ya ngazi zote inaweza kuidhinisha Kamati ya Utendaji katika ngazi husika kushughulikia kwa niaba ya shughuli maalumu ya shughuli zake na kamati husika shughuli hizo zitafanywa hivyo isipokuwa ngazi ya Taifa zitashughulikiwa na Kamati Kuu.

**Mikutano maalumu ya Chama ya Taifa**

5.5.29 Mkutano Mkuu Maalumu wa chama utaitishwa na Katibu Mkuu kwa maagizo ya Kamati Kuu ya chama au wajumbe wasiopungua theluthi moja wamekuwa na agenda maalumu na kupeleka maombi ya kuitishwa Mkutano Mkuu huo wa chama kwa taarifa isiyopungua siku 45. Maombi ya kuitisha Mkutano Mkuu huo wa chama ni lazima yatiwe saini na waombaji wote na kuambatana na Agenda kamili ya Mkutano huo.

**Wajumbe wa Kamati Kuu ya Chama:**

5.5.30 Mwenyekiti wa Chama.

5.5.31 Makamu wenyeviti Bara na Zanzibar
5.5.32 Katibu Mkuu
5.5.33 Manaibu Katibu Wakuu
5.5.34 Mkurugenzi wa fedha na Naibu wake

**Mwenezi na Naibu wake**

5.5.35 Wakuu wote wa Kurugenzi – Makao Makuu
5.5.36 Wajumbe wanne wataalamu wa fani mbalimbali walioteuliwa na Mwenyekiti wa Chama – Taifa kuingia kwenye Kamati Kuu.
5.5.37 Mwakilishi wa Wenyeviti wa mikoa atakayependekezwa na kamati kuu.
5.5.38 Kutakuwa na kamati ndogo Kamati Kuu – Zanzibar itakayoshughulikia masuala ya chama Tanzania Zanzibar ikiongozwa na Makamu Mwenyekiti Zanzibar. Kamati hii itatoa maamuzi yote kuhusu chama Zanzibar ambayo yataridhiwa au kutoridhiwa na Kamati Kuu – Taifa. Akidi ya vikao vya Kamati ndogo ya Kamati Kuu Zanzibar lazima viwe si chini 50% ya Wajumbe wote.

**Majukumu ya Kamati Kuu:**

5.5.39 Kujadili na kupendekeza kwa Mkutano Mkuu masuala yote yanayohusu Katiba ya chama na mabadiliko yake.
5.5.40 Kujadili na kupanga kanuni na taratibu za utawala, fedha, ajira na shughuli zote za chama.
5.5.41 Kubuni sera za Uchumi, Maendeleo ya Jamii na yote yanayogusia kila sekta na kuziwasilisha kwenye Mkutano Mkuu.
5.5.42 Kuandaa kwa kutumia Sekretarieti ya Kamati Kuu makala maalum za kitaalamu kuhusu sera za Taifa kwa majadiliano na uamuzi kwenye Mkutano Mkuu.
5.5.43 Kusimamia uchaguzi wa viongozi Wilayani na Mikoa
5.5.44 Kusikiliza na kutoa uamuzi unaohusu rufaa au mgogoro kutoka Mkoani, Wilayani au Matawini.
5.5.45 Kubuni na kupendekeza ilani ya uchaguzi kwa Mkutano Mkutano Mkuu.
5.5.46 Kuteua wakurugenzi wa Mkoa na Wilaya.
5.5.47 Uhalali wa Mkutano wa Kamati Kuu ni asilimia 50 ya wajumbe na uhalali wa maamuzi yake itakuwa kura zisizopungua asilimia 50 ya wajumbe wote waliohudhuria kikao hicho.
5.5.48 Mwenyekiti Taifa atapendekeza jina la Katibu Mkuu na Manaibu na kuyawasilisha kwenye Kamati Kuu. Kamati kuu ina mamlaka ya kukubali au kukataa mapendekezo ya M/kiti.
5.5.49 Mwenyekiti Taifa pia atapendekeza jina la Mkurugenzi wa Fedha na Naibu wake na kuyawasilisha kwenye Kamati Kuu. Kamati kuu ina mamlaka ya kukubali au kukataa mapendekezo ya M/kiti.
5.5.50 Kuchukua hatua za kinidhamu kwa kiongozi au mwanachama anayekiuka taratibu au Katiba ya Chama baada ya kumjadili na kuridhishwa na tuhuma zake.
5.5.51 Kamati Kuu inaweza kukaa kama kamati maalum ya chama ili kupitisha maamuzi ambayo yangepitishwa na Mkutano Mkuu wa Chama kama vile uteuzi wa mgombea Urais na Mwenza wake na mengineyo isipokuwa mabadiliko ya Katiba ya Chama.
5.5.52 Kamati Kuu ina uwezo wa kumsimamisha uongozi mwanachama yoyote na kusubiri maamuzi ya mwisho ya Mkutano Mkuu wa Chama.
5.5.53 Kuunda kurugenzi mpya kwa manufaa ya chama au kupunguza na kuridhia majina ya wajumbe watano walipendekezwa na Mwenyekiti wa Chama Taifa kuingia kwenye Kamati Kuu.

**Shughuli za Kamati Kuu**

5.5.54 Kusimamia na kuongoza shughuli zote za chama na kufanya mabadiliko ya Kanuni za uendeshaji wa Chama inapohitajika.
5.5.55 Kutekeleza maagizo ya Mkutano Mkuu na Mwenyekiti Taifa ndio msemaji Mkuu wa Chama.
5.5.56 Kufanya utafiti na kubuni sera
5.5.57 Kusimamia na kutekeleza sera za chama.
5.5.58 Kutekeleza kwa niaba ya Mkutano Mkuu shughuli zote zitakazoagizwa na Mkutano Mkuu.
5.5.59 Kuwasiliana na kujadiliana na Serikali kuhusu mambo yote yanayohusu maendeleo ya wananchi.
5.5.60 Kudumisha uhusiano mwema kati ya vyama vya siasa hapa nchini na vya nchi za nje.
5.5.61 Kubuni, kuendeleza na kuratibu shughuli za chama ili kudumisha uhusiano mzuri baina ya chama na Wananchi kwa kuwaelimisha juu ya sera na malengo ya chama.
5.5.62 Kuteua wajumbe wanne (wawili kutoka Zanzibar na wawili kutoka Bara) watakaoingia kwenye Kamati Kuu,.
5.5.63 Kuteua na kuajiri watumishi wa ngazi za Mikoa, Wilaya na Taifa.
5.5.64 Kamati Kuu ina uwezo wa kumsimamisha kiongozi yeyote na kukaimisha nafasi yake mpaka hapo rufaa yake itakapojadilwa kwenye Mkutano Mkuu.
5.5.65 Kutoa maamuzi ya mwisho kuhusu mapendekezo ya Kamati za Nidhamu za chama kuanzia Tawi hadi Taifa.

5.5.66 Kuteua wajumbe wa Bodi ya Wadhamini

5.5.67 Kamati Kuu ina uwezo wa kuteua Kamati mbalimbali kushughulikia masuala maalumu kama itakayoona inafaa.

5.5.68 Kila kamati itajiwekea utaratibu wa kutekeleza shughuli zake kufuatana na katiba hii.

5.5.69 Uhalali wa Kikao cha Kamati kuu itakuwa nusu ya wajumbe wote wa Kamati hii walioko Madarakani, Kamati itakutana kila inavyohitajika si chini ya mara moja ndani ya miezi mitatu na Mwenyekiti wa Chama Taifa anaweza kumualika na kumkaribisha Mwanachama yeyote kuhudhuria Mkutano huo lakini hatakua na haki ya kupiga kura.

**Muundo wa Sekretarieti ya Kamati Kuu**

**Sekretarieti itakuwa chini ya Katibu Mkuu atakayewajibika kwenye Kamati Kuu ya chama.**

5.5.70 Sekretarieti itakuwa na kurugenzi zifuatazo;-

(i) Kurugenzi ya Fedha na Uchumi
(ii) Kurugenzi ya Uenezi na Uchaguzi
(iii) Kurugenzi ya Katiba, Sheria, na Bunge
(iv) Kurugenzi ya Ulinzi na Usalama
(v) Kurugenzi ya Mahusiano na Jamii
(vi) Kurugenzi ya Habari na mawasiliano
(vii) Kurugenzi ya Miradi ya Chama
(viii) Kurugenzi ya Propaganda
(ix) Kitengo cha shughuli za wanawake
(x) Kitengo cha shughuli za vijana
(xi) Kitengo cha Wazee

**SHUGHULI ZA SEKRETARIETI**

1. Kuratibu utendaji wa kurugenzi zote pamoja na vitengo vya chama.
2. Kupendekeza na kuishauri Kamati Kuu kuhusu shughuli mbalimbali za Chama pamoja na kuandaa agenda za Kamati Kuu. Sekretarieti itakutana kila inapohitajika si chini ya mara moja kwa mwezi.

5.5.71 Wajumbe wa Sekretarieti ndio watakaoongoza kurugenzi na vitengo mbalimbali vya chama na watawajibika kutoa mapendekezo kuhusu utendaji ndani ya Chama kwa Katibu Mkuu wa Chama.

**KAMATI YA NIDHAMU**

5.5.72 Patakuwa na Kamati ya Nidhamu kuanzia ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa.

5.5.73 Wajumbe wa Kamati ya Nidhamu watakuwa (wasiozidi saba kila ngazi) watateuliwa na Mikutano Mikuu ya ngazi husika na kwa makao makuu watateuliwa na Kamati Kuu.

5.5.74 Shughuli za Kamati ya Nidhamu ni kushughulikia masuala yote ya nidhamu ndani ya chama na kupeleka ushauri, mapendekezo yake kwenye Kamati Kuu.

**IDADI WA WAJUMBE WA MKUTANO MKUU**

5.5.75 Kutokana na sababu za msingi kama vile ukata, kamati kuu inaweza kupunguza idadi ya wajumbe watakaohudhuria Mkutano Mkuu mradi uwepo uwiano wa uwakilishi wa wilaya, mikoa na jumuiya za chama.

## SURA YA NNE

## 6.0 UTARATIBU WA UCHAGUZI NA MIKUTANO

**Upendekezaji**

6.1 Mgombea wa wadhifa katika tawi lazima apendekezwe na wanachama wasiopungua wanne.

6.2 Mgombea wa wadhifa katika ngazi nyingine yoyote lazima apendekezwe na wajumbe wasiopungua watano.

**Kupiga kura:-**

6.3 Mgombea yeyote atachaguliwa iwapo atapata kura zaidi ya nusu ya kikao. Endapo pana mgombea mmoja tu, atapigiwa kura ya ndiyo au hapana iwapo kuna wagombea zaidi ya wawili na hakuna aliyepata kura zaidi ya asilimia 50, uchaguzi utarudiwa ukiwasilisha wagombea wawili waliopata kura nyingi zaidi.

6.4 Upigaji kura utakuwa wa siri.

6.5 Kiongozi wa chama na ngazi yoyote atashika wadhifa wake kwa kipindi cha miaka saba (7) na ana haki za kuchaguliwa tena.

**Kuacha Uongozi: -**

6.6 Kiongozi yeyote wa chama anaweza kusimamishwa wadhifa wake na Kamati Kuu ya chama kwa kura zaidi ya 50%.

6.7 Kiongozi yeyote wa Chama aliyechaguliwa anaweza kuondolewa katika wadhifa na Kamati Kuu na kumkaimisha mtu mwingine.

6.8 Kwa kujiuzulu

6.9 Kwa kiongozi kutohudhuria vikao vitatu vya ngazi husika kwa mfululizo bila kutoa udhuru au bila taarifa.

6.10 Kwa kushindwa kutimiza wajibu kwenye wadhifa wake au kuonyesha utovu wa nidhamu.

6.11 Nafasi yeyote ya kiongozi aliyechaguliwa inaweza kukaimishwa na kamati kuu ya chama mpaka hapo mkutano mkuu utakapofanyika.

## SURA YA TANO

### 7.0 MENGINEYO

**Mapato ya Chama yatatokana na :-**

7.1 Ada ya wanachama

7.2 Michango ya hiyari ya wanachama na watu wenye kukiunga chama mkono ndani na nje ya Tanzania

7.3 Mapato yoyote ya halali yatokayotolewa kwa chama

7.4 Misaada ya Ruzuku

7.5 Mapato yoyote ya halali yatokanayo na miradi ya chama

**Mali za Chama zitakuwa:-**

7.6 Mali zozote zenye kuondosheka na zisizoondosheka

7.7 Hisa katika miradi ya Chama au miradi ambayo Chama kina ubia

7.8 Kuwekwa benki katika hali ya kupata riba au katika hali ya hisa au namna yoyote ambayo Kamati Kuu ya Chama itaona kuwa ina manufaa kwa Chama

7.9 Kutumika kwa matumizi ya kawaida ya kukiendesha Chama na kuwekeza katika miradi ya Chama

7.10 Chama kitafungua akaunti benki katika jina lake katika kila ngazi kuanzia tawi hadi taifa.

### 8.0 KATIBA

**8.1 Marekebisho ya Katiba**

Taarifa ya mkutano wa kurekebishwa Katiba pamoja na mapendekezo ya marekebisho ni lazima yawasilishwe kwa wajumbe wote siku 30 kabla ya mkutano

**8.2 UTEKELEZAJI**

Kamati Kuu ya Chama itatengeneza kanuni za utekelezaji wa Katiba hii

### 9.0 WADHAMINI WA CHAMA, MSETO, WAASISI NA KUVUNJIKA KWA CHAMA

**9.1.1 BODI YA WADHAMINI**

9.1.2 Kutakuwa na wadhamini wa chama walioteuliwa na Kamati Kuu

9.1.3 Ardhi yote, majengo na mali yote ya kudumu, vitega uchumi na dhamana zitakapopatikana zitawekwa chini ya jina litakalosajiliwa na wadhamini hawa.

9.1.4 Wadhamini watateuliwa na Kamati Kuu kila baada ya miaka saba (7) na wanaweza kuchaguliwa tena. Wadhamini wanaweza kuacha udhamini kabla ya kipindi cha miaka saba kwa kujiuzulu au kuondolewa na kamati kuu kwa sababu ya makosa waliyofanya.

9.1.5 Kamati Kuu itaweka taratibu zitakazotumika kwenye Mikutano ya Baraza la Wadhamini

9.1.6 Mwenyekiti wa Chama Taifa ndiye Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini na Katibu Mkuu ndiye Katibu wa Bodi ya Wadhamini, Mkurugenzi wa fedha ndiye Mweka Hazina wa Bodi ya Wadhamini na ndiyo watakuwa wanaweka saini kwenye Akaunti ya wadhamini pamoja na mjumbe mwingine wa Bodi.

**9.2 Mseto**

9.2.1 Chama kinaweza kuunda mseto na chama chochote kile ambacho kinaweza kutimiza masharti yafuatayo: -

(a) Kinachoheshimu na haki ya msingi na uhuru wa Mtanzania

(b) Kinachojitolea kwa haki katika ushirikishaji wa Watanzania katika uongozi wa nchi.

(c) Chenye madhumuni na malengo yanayofanana na ya chama.

**9.3 Vitengo vya Chama: -**

9.3.1 Kitengo cha Vijana

9.3.2 Kitengo cha wanawake na Wazee

9.3.3 Umoja wa Wabunge / Wawakilishi wa Chama

9.3.4 Umoja wa Wabunge/Wawakilishi utaendeleza ushirikiano na Kamati Kuu na kwa makusudi haya utapeleka taarifa kwa Mkutano Mkuu juu ya mikakati ya shughuli zao.

9.3.5. Kama Mwenyekiti wa Chama siyo Mbunge, basi umoja wa Wabunge watamchagua mmoja wao kuwa kiongozi wa Umoja huo wa Wabunge.

**9.4 KUVUNJWA KWA CHAMA**

9.4.1 Chama kitavunjwa rasmi endapo robo tatu (¾) ya wajumbe wote watakaohudhuria mkutano mkuu wa chama wa Taifa ulioitishwa kwa madhumuni ya kuvunjwa kwa chama watapitisha hoja hiyo. Mkutano huo utatangaza rasmi kuvunjwa kwa chama na kusimamishwa kwa shughuli zote za chama.

9.4.2 Katika tukio la kuvunjwa cha chama bodi ya wadhamini wa chama itahodhi mali yote ya chama na kuitumia mali hiyo kulipia madeni yote ya chama. Endapo kutakuwa na salio lolote la mali ya chama baada ya kulipa madeni yote, Salio hilo litawasilishwa na kukabidhiwa kwa chama chochote cha wasiojiweza Tanzania kwa jinsi itakavyoamuliwa na Bodi ya Wadhamini.

9.4.3 Katika tukio la kuvunjwa kwa chama kwa nia ya kuungana na chama kingine cha siasa, bodi ya wadhamini wa chama itahodhi mali yote ya chama na kutumia mali hiyo kulipia madeni yote ya chama. Endapo kutakuwa na salio lolote la mali ya chama baada ya kulipa madeni ya chama, salio hilo litatumika kufuatana na Azimio la kuvunja chama ili kuungana na chama kingine.

**Imeridhiwa na Uongozi uliochaguliwa na Mkutano Mkuu tarehe 25/06/2010**

**Mwenyekiti wa Taifa** ..........................................................................

**Katibu Mkuu wa Taifa** ..........................................................................

25/06/2010